

**Baadhi ya majengo nane ya Hospitali ya Wilaya Namtumbo.** (Na Mpigapicha Wetu)

# Hospitali Wilaya ya Namtumbo ilivyo mkombozi kwa wajawazito

**Na Albano Midelo**

SERIKALI imekamilisha ujenzi wa majengo nane ya Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, ambapo kazi iliyokuwa imebaki, ya kuunganisha mfumo wa umeme na majisafi, imekamilika.

Kaimu Mganga Mkuu Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Dkt Godwin Luta, anasema kuwa halmashauri hiyo imekamilisha ujenzi wa hospitali ya wilaya, ambao umetokana na jitihada za serikali ya awamu ya tano, za kuhakikisha kwamba wakazi wanapata huduma za matibabu karibu na jirani na maeneo wanakoishi.

Serikali inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt John Magufuli, imedhamiria kuboresha utoaji wa huduma za afya kwa wananchi na kuwekwa msisitizo kwenye ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 ambapo hadi sasa vimejengwa vituo vya afya na hospitali katika maeneo mbalimbali nchini.

"Ujenzi huu umefanyika kwa awamu tano ambapo kwa mwaka 2010/2011, halmashauri yetu ilipokea fedha kutoka serikali kuu kiasi cha shilingi milioni 450 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na wagonjwa wa nje," Dkt Luta anasema.

Kwa mujibu wa daktari huyo, mwaka 2012/2013 halmashauri hiyo ilipokea fedha kutoka serikali kuu kiasi cha shilingi milioni 150 kwa ajili ya ujenzi wa kichomea taka, jengo la wodi ya wazazi, choo, kuweka umeme, mfumo wa majisafi na taka.

Mkuu wa Wilaya Namtumbo, Sophia Kizigo anasema kuwa katika utekelezaji wa ilani ya CCM kwa mwaka wa fedha 2018/2019, halmashauri ilipokea jumla ya shilingi bilioni 1.5 kutoka Ofisi ya Rais (TAMISEMI).

Anasema kuwa fedha hizo zilitolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa majengo nane ambapo hadi sasa zaidi ya shilingi bilioni 1.45 zimetumika na kiasi cha shilingi milioni 54 zilizobaki ambazo zimetumika kukamilisha mfumo wa majisafi na majitaka.

Kwamba, fedha hizo pia zimetumika kwa ajili ya barabara ya kupita wagonjwa, umeme na kuanzisha ujenzi wa jengo jipya la wodi ya watoto ambalo linatarajia kugharimu zaidi ya shilingi milioni 188.7.

Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya Namtumbo, Venance Nachimbinya, anabainisha zaidi kuwa kati ya fedha zilizotolewa, katika jengo la wodi ya wazazi zimetumika zaidi ya shilingi milioni 176 na jengo la wodi ya wanaume zimetumika zaidi ya shilingi milioni 259.

Anasema kuwa jengo la upasuaji limegharimu zaidi ya shilingi milioni 213, jengo la stoo ya dawa zaidi ya shilingi milioni 203, jengo la maabara milioni 164, jengo la kufulia zaidi ya milioni 113, jengo la mionzi zaidi ya milioni 136, jengo la wodi ya wanawake zaidi ya milioni 166 na jengo la watoto zaidi ya milioni10.

Nachimbinya anataja changamoto katika Idara ya afya kuwa ni uhaba wa watumishi na mabadiliko ya michoro kwa baadhi ya majengo, ikiwemo jengo la mionzi, wodi ya akinamama, wodi ya wanaume na jengo la upasuaji.

Mkurugenzi huyo, kwa niaba ya wakazi wa Halmashauri ya Namtumbo, anamshukuru Rais, Dkt John Magufuli, kwa jitihada kubwa za kuboresha huduma za afya kwa wananchi hali iliyofanikisha kukamilika kwa hospitali hiyo ya Namtumbo.

"Awali, kabla ya ujenzi wa hospitali hii, wananchi wa Namtumbo walikuwa wanasafiri umbali mrefu kutafuta huduma za afya, wakati mwingine walifuata huduma nje ya wilaya hasa wakinamama wajawazito na watoto," anasema Nachimbinya.

> *Awali, kabla ya ujenzi wa hospitali hii, wananchi wa Namtumbo walikuwa wanasafiri umbali mrefu kutafuta huduma za afya, wakati mwingine walifuata huduma nje ya wilaya hasa wakinamama wajawazito na watoto ...*
>
> **Venance Nachimbinya**
> Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya Namtumbo

Mary Mchucha ni mkazi wa Namtumbo, anaishukuru serikali kwa kukamilisha ujenzi wa hospitali ya wilaya ambayo anasema ni ukombozi kwa wanawake na watoto ambao kwa miaka mingi wamekuwa wanalazimika kusafiri umbali mrefu kutafuta huduma za afya.

"Baadhi ya wanawake wamekuwa wanapoteza maisha kwa kukosa huduma za afya katika maeneo ya jirani, lakini sasa hospitali hii imetukomboa, asante sana Rais wetu," Mary anasema.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma, Oddo Mwisho anasema kuwa alikuwa na kiu ya muda mrefu kuona wananchi wa Jimbo la Namtumbo wanapata hospitali ya wilaya iliyojengwa kwa viwango kulingana na mahitaji ili kusogeza huduma ya matibabu.

Anasema kuwa kwa miaka mingi wakazi wa Namtumbo wamepata kero kubwa ya kufuata matibabu mbali, hali ambayo imekuwa inawaathiri zaidi mama na mtoto na baadhi yao kupoteza maisha ambapo, amesema kwamba kukamilika kwa hospitali hii ni ukombozi kwa wanawake na wananchi wote kwa ujumla wake.

Hata hivyo, mwisho ameupongeza uongozi wa Halmashauri ya wilaya ya Namtumbo kwa kazi nzuri ya kusimamia mradi wa ujenzi wa hospitali ya wilaya ambapo anasema wananchi walikuwa na hamu kubwa ya kupata huduma bora zinazotolewa na hospitali hiyo.

Christina Mndeme, Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, anawaagiza watendaji wa halmashauri ya Namtumbo kuhakikisha kuwa majengo yaliyokamilika yanaanza kutumika kutoa huduma kwa wananchi wa Namtumbo ili kutimiza azma ya serikali ya kusogeza huduma ya afya karibu na wananchi.

"Wananchi hawataki kuona majengo. Badala yake wanataka kupata huduma za afya katika hospitali ,serikali imetekeleza wajibu wake wa kutoa fedha za kukamilkisha ujenzi," mkuu wa mkoa anasema.

John Milazi, mkazi wa Namabengo, anasema kuwa kutekelezwa kwa mradi huo kunamfanya ajisikie amani kwa sababu akinamama na watoto kwa miaka mingi walikuwa wanapata shida ambapo hivi sasa serikali imewakumbuka kwa kuwajengea hospitali yenye huduma zote muhimu.

Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo ilianzishwa mwaka 2002, ni kati ya halmashauri nane za Mkoa wa Ruvuma, ikiwa na eneo la ukubwa kilometa za mraba 20,375.1.

Kwa mujibu wa ofisi ya takwimu mkoa, Namtumbo ndiyo halmashauri yenye eneo kubwa kati ya halmashauri zote ambapo, hadi kufikia Septemba 2019 inakadiriwa ilikuwa na wakazi 229,142, kati yao wanaume wakiwa 112,103 na wanawake 117,039.

*• Mwandishi ni Afisa Habari Mkoa wa Ruvuma*

Scanned with CamScanner